





Siku moja Hamisi na babake walienda sokoni kununua sare ya shule.



Hamisi akamwona
kijana mwingine
amevalia shati la
kijani kibichi.
"Anaonekana
nadhifu sana,"
Hamisi aliwaza.



"Shati lile lapendeza sana," Hamisi alimwambia babake.



Hamisi aliendelea
kusema, "Tafadhali
baba, ninunulie
shati la kijani
kibichi."



"Hamisi, leo nitaweza kununua sare ya shule pekee." Baba alisema.



"Sina pesa za ziada za kukununulia shati kama hilo." Baba akaeleza.



Baada ya kulipia sare, baba alitambua kuwa alikuwa na pesa zilizobaki. Angeweza kumnunulia Hamisi shati la kijani kibichi!



Hamisi alifurahi sana. Alikimbia kwenda kujichagulia shati la kijani kibichi.